

NDOA BILA MAUMIVU.

Hali ya kushindwa kukabiliana na matarajio yasiyofikiwa; majeraha ya moyo, kushindwa kusamehe, kushindwa kuhimili taarifa mbalimbali ni miongoni mwa mambo ambayo huleta mipasuko ndani ya ndoa.

Kitabu hiki kimeelezea mambo muhimu yanayoweza kukusaidia kukabiliana na matarajio yasiyofikiwa, umuhimu wa kusamehe na mambo yanayoweza kukusaidia katika mchakato wa kusamehe, lakini pia kimeelezea namna unavyoweza kukabiliana na taarifa mbalimbali ili zisiwe chanzo cha maumivu na uharibifu kwenye ndoa.

Vile vile, kitabu hiki kimeeleza mambo mengine muhimu yanayoweza kukusaidia katika kuepuka maumivu ya mara kwa mara kama vile; namna ya kufanya mawasiliano sahihi, mambo muhimu ya kukusaidia katika kukabiliana na hasira, mambo ya kukusaidia kuwa mtu wa fikra chanya, nguvu ya maombi na mambo mengineyo muhimu yakuzingatia.

Kitabu hiki kimelenga kuwasaidia wanandoa na wanandoa watarajiwa ili kuweza kupata maarifa sahihi yatakayowasaidia kuepuka maumivu ya mara kwa mara na kujenga ndoa bora zenye ustawi.